Students Name: ……………………………………………………………………………

School Name…………………………………………… Index Number ……………

**P320/3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
Paper 3
Saa Tatu.
JULAI./AGOSTI

# HES MOCK EXAMINATIONS 2025

## UGANDA ADVANCED CERTIFICATE OF EDUCATION

## FASIHI YA KISWAHILI

### (RIWAYA)

### KARATASI YA TATU

### SAA TATU

**MAAGIZO**

- Karatasi hii ina sehemu A,B,CH, D
- Mtachiniwa anapaswa kujibu maswali matatu kwa ujumla
- Swali moja lazima litoke A na mengeni mawili yachaguliwe kutoka sehemu B, CH na D
- Mtahiniwa asichague maswali Zaidi ya moja kutoka sehemu moja

**SEHEMU A**

1. **UTENGANO: SAID A MOHAMED**

"………………….. hisi hakuwa kapoa kama ambavyo angalivyoopa hapo zamani. Zamani wakati kama huo angalipumbazwa na mandhari ya machuveo ya jua, na leo alikataa hata kupeleleza na wale popo waliokuwa wakitoka machokani kuja kula matunda karibu na nyumba yake hawakumfanya ainuke kwenda kuchukua bunduki yake kuwapiga.

Na sasa madmau jua linaanza kuzama, basi mbele yake Bi Tamima na binti yake Maimuna wangalikuwa kitahini wakichuma asumini vikuba na mawaridi. Almuradi manduavi hayo leo yalimkumbuisha yeye alikuwa nani kabla ya kujitawala, akawa nani baada ya kujitawala na leo yeye nani na kesho kutua atakuwaje hasa akiwa peke yake?

Hana mke wala watoto, ah, kama si yule lusu Tamina aliyewa…………………"

"lusu! Nani Lusu? Lusu Tamina au Maksuudi mwenyewe? Alijiuliza mwenyewe kwa mwenyewe. Alijitusi hana jawabu ya suala hili. Hakika walisema nia mbi huharibu nia njema tabu kweli wamesibu.Masuudi alijivuta kufikiri wakati ule aliposahau dhunia yake akajifanya bwana mbele ya umma. Hapo zamani angalijinyoosha hapo kwa kutafaraji. Pale pepo za magharibi zilipokuwa zikipuliza. Mbele ya nyumba yake na nyuma, kulia na kushoto, ilikuwa mali yake iliyoandikwa majina ya wanawe kwa kubabaisha. Alipalilia furaha ya maisha aishi maisha yasiyo taabu na atakapokufa watoto wake waje warithi.

Lakini furaha imegeuka msiba. Sasa hali yake imekuwa dhaifu. Jela imembomoa. Hali yake ihweza kutabirika. Na maisha ya wanawe asiyoyajua hatima yake, yote yamegubikwa na wingu kubwa linalongoja kuangusha dhoruba kali, nani aliyejua kuwa maksuudi atakuwa mzima leo, hivyo hivyo uzima wa olema, lakini bado anaishi? Lakini na iwe mali ya ujanja aliyonyanganywa, basi hata na watoto wake pia ulimwengu umenyanganya? Sasa amebakia kile kidogo kimekufa. Musa hakurejea tena kao toka siku aliyofumaniwa na babaake. Na maimuna, hayasemeki!

**MASWALI**

a) Jadili dondoo hili vikamilifu? (Alama 8)

b) Mwandishi anakusudia nini kulingana na, dondoo hili? (Alama 6)

ch)Fafanua hulka za mzungumzaji katika dondoo hili (Alama 4)

d) Ni maudhui yapi yanayojitokeza katika dondoo hii (Alama 6)

e) Jadili mbinu ya Sanaa iliyolitawala dondoo hili (Alama 6)

f) Dondoo hili lina manufaa gani kwa wasomaji wake (Alama 4)

2. **KIU: MOHAMED'S MOHAMED**

Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali kalamu yake ilitetemeka mkeneni ikingojea amri ya kutoka kichwani mwake……………… alipokuwa katika hali hii, alisikia hodi nje. Akifungua mlango na mara akaingia mtoto wa kiume mwenye uso wenye hata na nywele nyekundu ambazo labola hazikupata kuona kitana "shikamoo bwana" aliamkia huku akionyesha mkono wenye basua. Idi alikopokea barua kwa mshangao maana hakuwa akiazamia. Aligeuza upande wa pili akaona jina la bahati.

Barua ile iliwasha moto moyoni mwa iddi na kumchemsha kwa hasira ilimwia kama dhoruba kali ya ghafla. Mara macho yake yaligeuka rangi. Kipaji kikapetena na kidevu kika mwanguka, kwa ajabu na chungu. Alisoma tena ile barua na kila alopozidi kuisoma ndivyo alivyozidi ku chemka kwa hasira.

**MASWALI**

a) Nini kilitokea kabla ya dondoo (Alama 4)

b) Nini kilifuatia baada ya dondoo (Alama 4)

Ch)Jadili sifa za iddi katkia dondoo (Alama 6)

d) Fafanua mbinu zili zotumiwa Katika dondoo (Alama 4)

e) Taja hisia za iddi katika dondoo (Alama 4)

## SEHEMU B

3. a) Ni mafunzo yapi unayepata kama kijana kwa kurejelea riwaya hii. (Alama 21)

   b) Elezia namna mwanamke alivyochorwa katika riwaya, nguvu ya sala. (Alama 12)

4. a) Jadili mtindo wa lugha kama unajitokea katika riwaya hii.(Alama 17)

   b) Migogoro ni mojawapo ya matatizo yanayojitokeza katika tiwaya nguvu yasala. Tetea kauli hii. (Alama 16)

**BARAKA ZA MAMA: VINCENT M**

5. a) Jadili maudhui Baraka kama inavyojitokeza katika riwaya, Baraka za mama.

   (Alama 17)

   b) Unajifunza nini katika riwaya ya Baraka za mama. (Alama 16)

6. a) "Mabadiliko ni sehemu ya Maisha". Toa ukweli wa kauli hii kwa kurejea riwaya ya Baraka za mama. (Alama 17)

   b) Jadili mbinu za lugha kama zinavojitokeza katika riwaya ya Baraka za mama. (Alama 16)

## SEHEMU CH

**KUFA KUZIKANA: KEN.W.WALIBORA**

7. a) Jadili mbinu za lugha kama zinavyojitokeza katika riwaya ya Baraka za mama. (Alama 17)

   b) "Sihani zikiwa kwenye treya moja haziachi kugongana" dhihirisha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya kufa kuzikana. (Alama 33)

8. a) Kwa kutolea mifano mizuri kutoka riwaya ya kufa kuzikana, fafanua matatizo yaliyowakumba watu wa kiwachema. (Alama 17)

   b) urafiki baina ya akida na timu ni wa kufakuzikana. Jadili(Alama 16)

**UCHUNGU WA MWARIDI: NDANDA E ANTONY**

9. Jadili maudhui kama yanavyojitokeza katika riwaya ya uchungu wa Mwaridi. (Alama 33)

10. Fafanua masuala makuu yanayossisitizwa katika riwaya. (Alama 33)

## SEHEMU D

**UHASAMA KILIMANI: G.B MASEREKA**

11. Taswira ni mbinu pekee ina yotawa mchezo wa "uhasama kiliman". Jadili. (Alama 33)

12. a)Jadili maudhui katika riwaya hii (alama 17)

    b)Kwa kutolea mifano mwafaka eleza mivutasno inayo wakabili wahusika wa riwaya ya uhasama kilimani (Alama 17)

**JAHADA ZA FUA DAFU:WANYENYA WILLY**

13. Elimu na athari zake ndiyo maudhui pekee yanayojitokeza katika riwaya, "jitihada za fua dafu. Jadili. (Alama 33)

14. a)Jadili maudhui kama yanavyojitokeza katika riwaya ya jitihada za fua dafu. (Alama 16)

    b) Kwa kutolea mifano mwafaka,onyesha mandhari mbalimbali aliyoyatumia mwandishi katika riwaya. Jitihada za fua dafu!(alama 17)

**MWISHO**